# SAUTI YA TSC

TOLEO NA.8 JARIDA LA TUME YA UTUMISHI WA WALIMU TANZANIA (TSC) OKTOBA 2021

# TSC YATUMIA MILIONI 218 KUNUNUA PIKIPIKI KWA AJILI YA OFISI ZA WILAYA



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akikata utepe kwa ajili ya kugawa pikipiki kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC ngazi ya Wilaya Septemba 7, 2021 jijini Dodoma. Pembeni yake (mwenye miwani) ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akifuatiwa na Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Mwantum Zodo na upande wa kulia ni Kamishna wa TSC, Suzan Nussu.*

MAWASILIANO: Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
Simu: +255 (26) 2322402-4 Barua Pepe: secretary@tsc.go.tz Tovuti: www.tsc.go.tz

# PIKIPIKI ZA TSC ZITUMIKE KULETA TIJA KATIKA UTENDAJI KAZI WA OFISI ZA WILAYA

Hivi karibuni Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetumia kiasi cha shilingi milioni 218 kwa ajili ya kununua pikipiki 74 ambazo zimesambazwa kwenye ofisi za wilaya ikiwa ni moja ya njia ya kutatua changamoto ya usafiri katika ofisi hizo.

Pikipiki hizo zilikabidhiwa kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu Septemba 7, 2021 ambapo alisisitiza kuwa vyombo hivyo vitumike kwa ajili ya kuleta mabadiliko ya utendaji wa kazi katika ofisi za wilaya.

Kwa kuwa pikipiki hizo ni chache ikilinganishwa na idadi ya ofisi za TSC katika wilaya zote za Tanzania Bara, Menejimenti ya Tume iliamua kupeleka vyombo hivyo kwenye wilaya zenye changamoto zaidi katika kuwafikia walimu.

Hivyo ni vyema kila ofisi iliyopewa chombo hicho cha usafiri kuelewa kwamba vyombo hivyo vinatumika katika kutimiza malengo ya serikali ya kuboresha huduma kwa walimu, haitarajiwi hata kidogo kuona vyombo hivyo vikitumika kwa matumizi mengine kinyume na utaratibu.

Ni matarajio yetu kuwa Uongozi wa Tume chini ya Katibu wake, Paulina Nkwama utahakikisha unatoa huduma inayostahiki kwenye vyombo hivyo ikiwa ni pamoja na mafuta na matengenezo kwa kadri inavyohitajika ili viweze kutumika wakati wote.

## BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Paulina Nkwama

**Wajumbe**
Moses Chitama
Christina Hape
Richard Odongo
Revocatus Misonge
Mectildis Kapinga
Lameck Mbeya

**Mhariri Mkuu**
Gerard Chami

**Mhariri**
Adili Mhina

**Msanifu Kurasa**
Lucas Gordon

## KATUNI




**Wasiliana nasi kwa Simu:** +255 782 366 622 & +255 735-255238 **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz*
Au fika Ofisi ya Mawasiliano, Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mtaa wa Mtendeni, ***S.L.P 353, DODOMA.***

# TSC YATUMIA MILIONI 218 KUNUNUA PIKIPIKI KWA AJILI YA OFISI ZA WILAYA



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akiwa amekabidhi pikipiki kwa mmoja wa Watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya ikiwa ni ishara ya kukabidhi pikipiki 74 kwa ofisi mbalimbali za TSC Wilaya.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akiongea na watumishi wa TSC (hawapo pichani) wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki 74 kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC ngazi ya Wilaya.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Paulina Nkwama akitoa neno fupi mbele ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Seikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki 74 kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi TSC ngazi ya Wilaya iliyofanyika Septemba 7, 2021 Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu.**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imetumia kiasi cha shilingi milioni 218 kwa ajili ya kununua pikipiki 74 ambazo zimesambazwa kwenye ofisi za wilaya kwa lengo la kutatua changamoto ya usafiri kwa watumishi wake katika kutoa huduma kwa walimu.

Akikabidhi pikipiki hizo kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC kutoka Wilaya mbalimbali mapema mwezi Septemba 2021, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mhe. Ummy Mwalimu aliipongeza TSC kwa hatua hiyo na kusema itasaidia watumishi hao kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.

Waziri Ummy alisema kuwa TSC ni chombo muhimu katika kusimamia utumishi wa walimu

# TSC YATUMIA MILIONI 218 KUNUNUA PIKIPIKI KWA AJILI YA OFISI ZA WILAYA



*Mbunge wa Jimbo la Wingwi na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Omar Issa Kombo akitoa neno fupi wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki kwa watumishi wa TSC ngazi ya Wilaya.*



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) Suzan Nussu akitoa neno kwa niaba ya Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi TSC ngazi ya Wilaya iliyofanyika Septemba 7, 2021 Dodoma.*

hivyo ni jambo la busara kutoa vyombo vya usafiri kwa maafisa wake wa wilayani ili waweze kutembelea walimu na kutatua changamoto zao kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu nchini.

"Nakupongeza sana Katibu pamoja na viongozi wote wa TSC kwa kuona umuhimu wa kuwapatia vyombo vya usafiri watumishi wenu wa wilayani. Watumishi hawa ndiyo wenye jukumu kubwa katika kutekeleza malengo ya Tume na Serikali kwa ujumla kwa kuwa wao ndio wako na walimu wakati wote, hivyo kuwapatia pikipiki hizi kutawawezesha kutembelea shule kwa urahisi", alisema Waziri Ummy.

Kiongozi huyo aliwataka Kaimu Makatibu Wasaidizi wa




*Baadhi ya pikipiki zilizonunuliwa na TSC kwa ajili ya Ofisi za Wilaya. Pikipiki hizo zilikabidhiwa na Waziri wa TAMISEMI, Mhe. Ummy Mwalimu (MB) kwa Katibu wa TSC ngazi ya Wilaya, Septembe 7, 2021.*

# TSC YATUMIA MILIONI 218 KUNUNUA PIKIPIKI KWA AJILI YA OFISI ZA WILAYA



*Baadhi ya Watumishi wa TSC wakiwa katika hafla ya kukabidhi pikipiki kwa Katibu Wasaidizi TSC ngazi ya Wilaya.*

"Simamieni maadili na nidhamu, ni wajibu wenu kuhakikisha heshima ya kada hii haishuki, vilevile lazima tukumbuke kuwa tuna watoto ambao lazima tuwalinde wakati wote. Wale walimu wachache ambao sio waadifu tusiwavumilie hata kidogo" amesema Ummy.

Waziri Ummy ameendelea kusema kuwa TSC ina wajibu wa kuhakikisha wanawasikiliza walimu kwa karibu na kutatua changamoto zao kwa wakati ili walimu waendelee kuwa na moyo wa kufanya kazi kwa bidii na kwa kujituma.

Tume kuhakikisha vitendea kazi hivyo vinatumika kwa masuala ya utekelezaji wa majukumu ya kila siku na zisigeuzwe kuwa vyombo vya kufanyia biashara ya kubeba abiria (bodaboda).

Aidha, Waziri Ummy amewataka Kaimu Makatibu hao kuendelea kusimamia kwa weledi kada ya walimu kwa kuwa ndio wenye jukumu kubwa la kuandaa taifa linaloweza kufikia malengo yake katika masuala ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

Pamoja na hayo, Waziri huyo amesisitiza kuwa ili kulinda hadhi ya kada ya ualimu pamoja na kulinda haki za wanafunzi, ni lazima TSC ichukue hatua za kinidhamu kwa walimu wanaokiuka maadili hasa wale wanaojihusisha na mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Seikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) (katikati) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Watumishi wa TSC kutoka Wilaya mbalimbali wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki 74 kwa watumishi hao. Pichani, waliokaa ni Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Mwantum Zodo (wa kwanza kushoto) akifuatiwa na Mbunge wa Jimbo la Wingwi na mjumbe wa Kamati hiyo, Mhe. Omar Issa Kombo. Wengine ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama (wa pili kutoka kulia) na Kamishna wa TSC, Suzan Nussu (wa kwanza kutoka kulia).*

# WAKUU WA SHULE WATAKIWA KUSIMAMIA ELIMU, FEDHA ZA MIRADI KWA UFANISI

**Na Mwandishi Wetu.**

Wakuu wa Shule wametakiwa kusimamia kwa ufanisi utoaji wa elimu kwa wanafunzi na fedha za miradi zinazotolewa na Serikali kwa ajili ya kujenga na kuboresha miundombinu ya shule mbalimbali nchini.

Maelekezo hayo yametolewa Septemba 14, 2021 na Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe wakati akifungua Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe akitoa hotuba ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli akitoa neno la kumkaribisha Katibu Mkuu TAMISEMI (hayupo pichani) ili afungue Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma hivi karibuni.*

Alisema kuwa walimu wa shule za msingi ni nguzo kubwa katika kuandaa taifa imara kwani elimu ya msingi ndiyo inayoweza kuamua mtoto awe raia mzuri anayeweza kuwa na mchango chanya katika maendeleo ya taifa lake au la.

Hivyo, ili kuandaa raia wema, wenye ujuzi, wachapakazi na wazalendo ni lazima walimu wa shule za msingi kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kutoa elimu bora kwa wanafunzi, jukumu ambalo Katibu Mkuu anawataka wakuu wa shule kulisimamia wakati wote na kuhakikisha linatekelezwa vizuri.

"Ninawasihi sana walimu tuendelee kushirikiana ili tuwasaidie wanafunzi wetu, mwalimu wa shule ya msingi asipofanya kazi yake vizuri taifa haliwezi kwenda popote. Mimi nisingekuwa hapa kama nisingefundishwa vizuri nikiwa shule ya msingi hivyo kila mmoja wenu ahakikishe anatekeleza wajibu huo kama inavyotakiwa kwa manufaa ya Taifa letu," alisema Prof. Shemdoe.

Akisisitiza suala la walimu kutimiza wajibu wao, Kiongozi huyo amewataka walimu kutojiingiza katika vitendo vya udanganyifu wa mitihani kwani kufanya hivyo sio kwamba tu ni kinyume na maadili ya kazi ya ualimu lakini pia kinarudisha nyuma maendeleo ya Taifa.

Alieleza kuwa hata kama mwalimu atalazimishwa na mkuu wake wa kazi au kushawishiwa na wazazi ili awasaidie wanafunzi wakati wa mtihani kinyume na sheria, kanuni na taratibu asikubali na badala yake atoe taarifa kwenye vyombo vinavyohusika ili sheria iweze kuchukua mkondo wake.

"Juzi tu tulikuwa kwenye mitihani ya Darasa la Saba, zipo kesi chache zilizojitokeza kuhusu udanganyifu wa mititihani. Ninawasihi walimu msikubali

# WAKUU WA SHULE WATAKIWA KUSIMAMIA ELIMU, FEDHA ZA MIRADI KWA UFANISI



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akifuatilia hotuba ya Katibu Mkuu TAMISEMI (hayupo pichani) wakati wa ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma hivi karibuni.*



*Mkurugenzi Msaidizi anayesimamia Elimu ya Awali na Msingi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambaye pia ni Kamishna wa TSC, Suzan Nussu akimuonesha jambo Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli wakati wa Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma hivi karibuni.*

kuingia katika mtego huo, kuna maeneo mnaweza kujikuta mnashawishiwa na wazazi au hata viongozi wenu wa kazi, msikubali. Ukiona kuna jambo la namna hiyo wewe tupatie taarifa hata kama ni kwa siri sisi tutajua namna ya kushughulika nalo," alisema Shemdoe.

Kuhusu usimamizi wa fedha za miradi ya maendeleo shuleni, kiongozi huyo alieleza kuwa wakuu wa shule wanapaswa kuzingatia sheria kanuni, taratibu, miongozo na maelekezo yanayotolewa na Serikali katika kutekeleza miradi




*Baadhi ya wanachama wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) wakisikiliza hotuba ya ufunguzi wa mkutano wa tatu wa chama hicho kutoka kwa Katibu Mkuu TAMISEMI (hayupo pichani) jijini Dodoma.*

# WAKUU WA SHULE WATAKIWA KUSIMAMIA ELIMU, FEDHA ZA MIRADI KWA UFANISI



*Baadhi ya wanachama wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) wakiwa katika hali ya furaha wakati wa mkutano huo uliofanyika jijini Dodoma hivi karibuni.*

hiyo ili wajiepushe na matatizo yanayoweza kutokea pale taratibu zinapokiukwa.

“Serikali inatoa fedha kwa ajili ya miradi ya shule hususan ujenzi wa madarasa, usipokuwa makini fedha hizi zitakunyang’anya madaraka uliyonayo sasa, zitakufukuzisha kazi au kukufunga jela. Sitamani kuona mmoja wenu anaingia kwenye matatizo kutokana na kushindwa kutimiza wajibu wake aliopewa katika kusimamia miradi ya shule. Hivyo simamieni miradi hiyo kwa weledi, maarifa na uzalendo kwa kuzingatia sheria,” alisema.

Akimalizia hotuba yake, Katibu Mkuu huyo aligusia Suala la chanjo ya Ugonjwa wa Virusi vya Korona (UVIKO-19) ambapo aliwaeleza walimu hao kuwa kwa kuwa suala la kuchanja ni la hiari, ni vizuri kwa wale ambao bado hawajachanjwa wafike kwenye vituo vinavyotoa huduma ya chanjo ikiwa ni njia mojawapo ya kuwahamasisha watumishi walio chini yao na jamii inayowazunguka kupata chanjo.

“Ninyi ni viongozi na sio kwamba mnaaminiwa tu na




*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya Wanachama wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA).*

# WAKUU WA SHULE WATAKIWA KUSIMAMIA ELIMU, FEDHA ZA MIRADI KWA UFANISI



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe akiwa na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama pamoja na walimu (wenye flana nyekundu) mara baada ya ufunguzi wa Mkutano wa TAPSHA jijini Dodoma.*

walimu mnaowaongoza lakini pia hata wanajamii huko kwenye maeneo yenu wanawaamini. Kuna watu wengi wanawaangalia ninyi kuwa mnafanyaje na wanaamini kile mnachofanya ndiyo sahihi. Kama mkienda kupata chanjo mtaona na wao wanakwenda kuchanja. Hivyo ninawasihi mtumie uhuru uliotelewa vizuri kwa kuchagua lile lililo jema kwa ajili ya kulinda afya zetu," alisema.

Mkutano huo uliofanyika kwa siku tatu na wenye kaulimbiu 'usimamizi thabiti wa taaluma, Tehama na miradi ya maendeleo ni chachu katika utoaji wa elimu bora', ulihudhuriwa na viongozi wengine wakiwemo Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama pamoja na Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu ya Awali na Msingi TAMISEMI ambaye pia ni Kamishna wa TSC, Suzan Nussu.



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe (kulia) akifurahia jambo na Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli (kushoto) pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*



*Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe akiagana na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama baada ya ufunguzi wa Mkutano Mkuu wa Tatu wa Umoja wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi Tanzania Bara (TAPSHA) uliofanyika katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma hivi karibuni.*

# Spika Ndugai apongezwa kwa kutoa Msaada wa Pikipiki TSC Kongwa

**Na. Mwandishi Wetu.**

Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa, Job Ndugai amepongezwa kwa kuunga mkono juhudi za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika kutoa huduma bora kwa walimu.

Mhe. Ndugai amepata pongezi hizo baada ya kutoa msaada wa pikipiki moja kwa ofisi ya TSC Wilaya ya Kongwa ili iweze kusaidia maafisa wa Tume hiyo kutembelea walimu, kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili kwa lengo la kuboresha sekta ya elimu nchini.

Pongezi hizo zimetolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. Ummy Mwalimu (Mb) pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki 74 zilizonunuliwa na Tume hiyo kwa ajili ya ofisi zake za wilayani.

Katika hafla hiyo iliyofanyika mapema mwezi Septemba katika ofisi za TSC Makao Mkuu jijini Dodoma, Waziri Ummy alieleza kuwa Mhe. Ndugai amefanya jambo linalopaswa kuigwa na kila kiongozi katika kuchangia maendeleo ya elimu nchini.

Aliongeza kuwa Pikipiki hiyo itasaidia maafisa wa Tume katika wilaya hiyo kufanya ziara katika shule mbalimbali hususan zile za pembezoni ambapo hakuna usafiri wa uhakika.

"Napenda kumpongeza sana Mhe. Ndugai kwa kutoa msaada wa pikipiki katika ofisi ya TSC wilayani Kongwa. Pikipiki hiyo itasaidia kuongeza kasi ya utoaji huduma kwani watumishi wana uhakika wa usafiri pale wanapotaka kutembelea walimu. Natamani viongozi wengine tuige mfano wa Mhe. Ndugai katika kuisaidia TSC iweze kuhudumia walimu kwa ufanisi zaidi," alisema Waziri Ummy.

Akitoa maelezo ya utangulizi wakati wa hafla ya kukabidi pikipiki hizo, Katibu wa TSC Paulina Nkwama alisema TSC ina changamoto kubwa ya vyombo vya usafiri hususan katika ofisi za wilaya hivyo, pale wadau wanapojitokeza na kutoa msaada inarahisisha utendaji kazi katika kuwahudumia walimu.

"Mh. Waziri kwa kweli Tume imefurahishwa sana kwa kitendo cha Spiga wetu wa Bunge kuamua kutoa msaada wa pikipiki katika ofisi yetu ya Kongwa. Kama unavyojua TSC ni Taasisi ambayo imeanza kufanya kazi mwaka 2016 na tuna ofisi katika Wilaya zote hapa Tanzania Bara, Bado hatujajitosheleza katika mambo mengi, lakini linalotusumbua sana kwa sasa ni suala la usafiri, ndiyo maana tumeamua kununua pikipiki 74 ambazo utazikabidhi leo ili zikasaidie kwenye ofisi zetu huko wilayani," alisema Nkwama.



*Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa, Mhe. Job Ndugai.*

# TSC YATAKIWA KUFANYA UFUATILIAJI WA MSAWAZO WA WALIMU



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akiongea na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi (hawapo pichani) wakati akifungua mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dodoma.*

**Na Mwandishi Wetu**

Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imeagizwa kufanya ufuatiliaji wa msawazo wa walimu katika shule za msingi na sekondari za serikali ili kuhakikisha uwepo wa uwiano sawa wa walimu wa shule za mjini na zile za pembezoni.

Agizo hilo limetolewa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu wakati akifungua Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi la TSC ulilofanyika Septemba 9, 2021 katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango, jijini Dodoma.

Waziri Ummy alieleza kuwa kuna wimbi kubwa la walimu wanaofundisha shule za vijijini kutaka kuhamia mjini na kuacha shule hizo bila walimu kitu kinachowanyima wanafunzi haki ya kufundishwa, hivyo ameitaka TSC kufanya ufuatiliaji ili kuona hali ya msawazo wa walimu kwa shule za mjini na vijijini.

"Ndugu Katibu wa Tume, kwa mujibu wa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu Sura 448, jukumu la kuhakikisha kunakuwa na msawazo sawa wa walimu lipo kwenu TSC. Hivyo nataka mfanye ufuatiliaji kuona hali ya walimu kwa kubainisha walimu wanaohitajika, waliopo na upungufu wao kwa kila halmashauri. Taarifa hiyo niipate ndani ya wiki mbili ili tuweze kuchukua hatua stahiki," alisema Waziri Ummy.

Waziri alifafanua kuwa shule za pembezoni zina upungufu mkubwa wa walimu lakini bado walimu wanataka kuhama wakati shule nyingi za mjini walimu wapo na wakati mwingine wanagawana mada za kufundisha kwenye somo moja.

"Kuna maeneo ya vijijini



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa maelezo ya awali wakati wa Baraza la Wafayakazi la TSC Septemba 9, 2021, Dodoma.*

# TSC YATAKIWA KUFANYA UFUATILIAJI WA MSAWAZO WA WALIMU



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi na viongozi wengine mara baada ya kufungua mkutano wa baraza hilo Septemba 9, 2021, jijini Dodoma. Pichani, kushoto kwa Waziri ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama.*

unakuta darasa la kwanza hadi la saba kuna walimu watatu na hao wanatakiwa kufundisha wanafunzi wote. Lakini ukija shule za mijini unakuta somo moja linafundishwa na walimu watatu hii siyo sawa," alisema Mhe. Ummy.

Kutokana na hali hiyo, Waziri Ummy amezielekeza mamlaka zinazohusika na uhamisho wa walimu kutofanya uhamisho wa mwalimu yeyote kutoka shule za pembezoni kuja mjini kabla ya kupeleka mwalimu kujaza nafasi ya anayehama.

"Wanafunzi wa vijijini wanahitaji kupata elimu kama walivyo wa mijini, sasa tukiachia tu kila mwalimu anayetaka kuondoka shule aondoke shule za vijijini zitabaki bila walimu. Hivyo ninaelekeza kuwa ni marufuku kumhamisha mwalimu kutoka pembezoni kwenda mjini kabla ya kupata mwalimu wa kujaza nafasi ya anayehama," alieleza Waziri Ummy.

Alifafanua kuwa marufuku hiyo haimaanishi kuwa amefuta uhamisho wa walimu lakini kinachotakiwa ni kupatikana kwa mwalimu anayehamia kijijini kabla ya anayetaka kwenda mjini kuhama.

Hata hivyo, Waziri alieleza kuwa kwa mwalimu yeyote anayetaka kuhama kutoka mjini kwenda maeneo ya pembezoni apatiwe uhamisho huo ndani ya muda mfupi ili akaongeze nguvu huko ambako kuna walimu wachache zaidi.

"Kwa hili nitakuwa mkali sana. Sio kwamba nimekataza uhamisho wa walimu, ninachotaka hapa ni kuhakikisha shule za pembezoni nazo zinakuwa na walimu wa kutosha. Hivyo, mwalimu anayetaka kutoka mjini kwenda pembezoni huyo hatuna shida naye, apewe uhamisho wake mara moja aende akatusaidie huko", alisisitiza Waziri Ummy.

Aliongeza kuwa badala ya kukaa maofisini ni vyema zikafanyika ziara za ufuatiliaji wa utoaji elimu, ukaguzi wa mazingira ya makazi ya walimu na miundombinu pamoja na kutoa elimu zaidi juu ya maadili, miiko



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika Mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

# TSC YATAKIWA KUFANYA UFUATILIAJI WA MSAWAZO WA WALIMU



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika Mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

na nidhamu katika utumishi wa walimu na utumishi wa umma.

Waziri huyo pia akieleza kuwa TAMISEMI kwa kushirikiana na TSC kuandaa Mwongozo wa Walimu wanaojitolea kufundisha shule za msingi na sekondari za serikali ili kuwatambua na kuwatendea haki pale nafasi za ajira zinapotolewa na Serikali.

Pamoja na hayo Waziri Ummy alitoa pongezi kwa Tume kutofumbia macho walimu wanaokutwa na makosa hasa utoro kazini, pia alielekeza kuwa kwa kuanzia, shule zilizopo kwenye Majiji ya Dar es Salaam, Arusha, Mbeya na Tanga zifungwe vifaa vya kielektroniki (Biometric) kwa ajili ya kuchukua mahudhurio ya walimu ili kudhibiti utoro na uchelewaji kazini kwa walimu.

Pia, liwahakikishia Wajumbe wa Baraza la TSC kuwa atapambania ongezeko la bajeti ya Tume wakati utakapowadia wa maandalizi ya bajeti ikiwa ni baada ya kupata vipaumbele mahsusi vitakavyosaidia kujenga hoja za kushawishi kupata ongezeko hilo.

Naye Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa maelezo ya utangulizi alisema, Tume kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI imefanikiwa kwa hatua za awali kujenga Mfumo wa Kielektroniki ujulikanao kama Teachers Service Commission Management Information System (TSCMIS) kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya Tume, hatua za ujenzi wa Mfumo huo zimekamilika na Moduli tatu (3) kati ya sita (6) zimefanyiwa majaribio.

Vilevile, alisema kuwa katika jitihada za kukabiliana na changamoto ya ukosefu wa jengo la ofisi Makao Makuu, Tume imefanikiwa kununua kiwanja eneo la Chinyoya - Ntyuka, Dodoma, chenye ukubwa wa mita za mraba 3,348 ambapo katika Mwaka wa Fedha 2021/22 Tume ilitenga na imepokea fedha kiasi cha shilingi milioni 500 mwezi Julai, 2021 kati ya Shilingi Bilioni 3.9 zinazohitajika kukamisha ujenzi huo.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (kulia) akizungumza jambo na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama mara baada ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

# TSC kushughulikia Watumishi wake wanaojihusisha na Rushwa

**Na Mwandishi Wetu**

Katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewapandisha vyeo walimu 126,346 na kati yao walimu 121,663 sawa na asilimia 96.2 wabebadilishwa mishahara yao kutoka ile ya vyeo vya zamani kwenda katika vyeo vipya.

Zoezi la kuwapandisha vyeo walimu linahusisha kwa karibu Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri pamoja na Ofisi ya TSC katika Wilaya husika ambapo mwajiri anawasilisha mapendekezo ya walimu wanaotakiwa kupandishwa, Katibu Msaidizi anafanya




*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli akitoa hotuba ya kufungua Mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringia yaliyofanyika Septemba 20 na 21 katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akitoa neno la kumkaribisha Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI anayeshughulikia Elimu, Gerald Mweli (Hayupo pichani) ili afungue Mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringia yaliyofanyika Septemba 20 na 21 katika Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*




*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akitoa maelezo ya awali wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

# TSC kushughulikia Watumishi wake wanaojihusisha na Rushwa

uchambuzi na kuwasilisha mapendekezo hayo kwenye Kamati ya TSC ngazi ya Wilaya kwa ajili ya Uamuzi na kisha Katibu Msaidizi anawaandikia walimu barua za kupanda cheo.

Kwa mujibu wa wadau mbalimbali wakiwemo walimu wenyewe, zoezi la upandishaji vyeo watumishi wa umma wakiwemo walimu lililofanyika miezi michache iliyopita lilitekelezwa kwa ufanisi mkubwa ikilinganishwa na miaka iliyopita.

Kauli hiyo inaungwa mkono na Naibu Katibu Mkuu kutoka Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli ambaye anaipongeza TSC kwa kusimamia zoezi hilo kwa weledi na kufanya asilimia 96 ya walimu waliopandishwa madaraja kubadilishiwa mishahara.

Hata hivyo, Naibu Katibu Mkuu huyo anaeleza kuwa pamoja na zoezi hilo kufanyika kwa ufanisi zipo changamoto zilizojitokeza ambapo baadhi ya watendaji wanalalamikiwa kujihusisha na vitendo vya rushwa ili kutoa upendeleo kwa baadhi ya walimu ambao hawakuwa na sifa za kupanda vyeo huku wenye sifa wakiachwa.

Kutokana na changamoto hiyo, Naibu Katibu Mkuu Mweli ameiagiza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), kufanya tathmini ya wazi katika zoezi la upandishaji vyeo walimu lililofanyika hivi karibuni ili kubaini kama kila mwalimu aliyestahili kupandishwa cheo amepata haki hiyo.

Mweli ametoa agizo hilo Septemba 20, 2021 wakati akifungua mafunzo ya siku mbili yaliyowakutanisha wajumbe wa Kamati za TSC ngazi ya Wilaya kutoka katika Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Iringa na Manyara yanayofanyaika kwa siku mbili katika Chuo cha Mipango, Dodoma.

Kiongozi huyo ameeleza kuwa yapo malalamiko kuwa baadhi ya watumishi wasio wa adilifu walitumia vibaya mamlaka waliyonayo katika kupandisha vyeo walimu na kujihusisha na vitendo vya rushwa kitu ambacho kimesababisha baadhi ya walimu




*Mkurugenzi wa Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Christina Hape akiwasilisha mada kuhusu historia ya TSC katika mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*




*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu kutoka TSC, Moses Chitama akiwasilisha mada juu ya Muundo wa Tume hiyo katika mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

# TSC kushughulikia Watumishi wake wanaojihusisha na Rushwa



*Mkurugenzi Msaidizi wa Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Mecktildis Kapinga akiwasilisha mada juu ya majukumu ya TSC katika kushughulikia Ajira na Maendeleo ya Walimu katika mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*



*Mkurugenzi Msaidizi Maadili na Nidhamu kutoka TSC, Robert Lwikolea akitoa mada kuhusu Maadili ya Kazi ya Ualimu katika mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

kukosa haki yao ya kupandishwa madaraja.

"Natambua kazi kubwa ambayo inafanywa na TSC hasa katika zoezi la kupandisha madaraja walimu. Lakini pamoja na kazi hiyo zipo changamoto ambazo tumeziona wakati wa utekelezaji wa zoezi hilo. Wapo baadhi ya Kaimu Katibu Wasaidizi ambao wanatuhumiwa kwa rushwa. Ninahitaji mfanye tathmini katika Wilaya zote muone namna zoezi hilo lilivyokwenda," aliesema Mweli.

Alisisitiza kuwa anataka tathmini hiyo iwe na vigezo vya wazi ili kuona kama kila mwalimu aliyekuwa na sifa za kupanda daraja amepandishwa na kama kuna ambao hawakuwa na sifa lakini wamepandishwa ili hatua stahiki zichukuliwe kwa watumishi wote waliokiuka utaratibu uliotolewa.

"Hapa ukitaka kufuatilia suala la rushwa inaweza ikawa ngumu kuthibitisha moja kwa moja lakini tukiweka vigezo vya wazi tutapata majibu. Kama utakuta mwalimu hana sifa lakini kapandishwa na mwenye sifa hajapandishwa, ni wazi kuwa kuna mchezo umefanyika na lazima tuchukue hatua", alisisitiza Naibu Katibu Mkuu.

Ameeleza kuwa kunapokuwa na baadhi ya watendaji ambao sio waadilifu, sio tu kwamba wanawakosesha walimu haki zao bali pia inachafua taswira ya Tume ya Utumishi wa Walimu na kusababisha chombo hicho kukosa heshima na kutoaminiwa na jamii.

"Anapotokea mtumishi mmoja kati yenu akajihusisha na rushwa matokeo yake ni kwamba TSC yote inaonekana kuwa ni ya wala rushwa. Hivyo Katibu wa Tume, hili naomba tulikemee kwa nguvu zote ili walimu waweze kuhudumiwa kwa haki kwa kuzingatia sheria," alieleza Mweli.

Akizungumzia kuhusu mafunzo hayo, Mweli alisema kuwa Kamati za Wilaya zinaundwa na wajumbe wenye taaluma tofauti tofauti na wanatakiwa kushughulika na masuala ya utumishi wa walimu, hivyo ni muhimu wapatiwe mafunzo ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

"Niwapongeze sana TSC kwa kuona umuhimu wa kufanya mafunzo haya kwa kuwa hizi kamati za wilaya ndizo hasa zinazotekeleza majukumu ya

# TSC kushughulikia Watumishi wake wanaojihusisha na Rushwa



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Kamati za TSC za Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

msingi ya Tume. Hivyo ili waweze kufikia matarajio mnayoyataka ni lazima muwajengee uwezo wa namna ya kufikia malengo hayo. Baada ya mafunzo haya watakapoboronga mna haki ya kuwauliza kwa kuwa tayari mmewawezesha," alieleza.

Naye Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba alisema kuwa TAMISEMI imekuwa na ushirikiano wa karibu sana na TSC na hivyo imeisaidia Tume hiyo kutatua changamoto mbalimbali zilizokuwa zinaikabili hususan katika ofisi zake za wilayani.

"Ndugu Naibu Katibu Mkuu sisi tunakushukuru wewe binafsi pamoja na ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ushirikiano mkubwa ambao tunaupata kutoka kwenu. Mmesaidia watumishi wetu wa wilayani kupata ofisi kwa Wakurugenzi na mmekuwa mkitusaidia kwenye masuala ya miundombinu



*Kamishna wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) anayewakilisha shule za sekondari, Jane Mtindya akiongea na wajumbe wa mafunzo ya Kamati za TSC (hawapo pichani), pembeni yake ni Kamishina wa TSC anayewakilisha shule za msingi, Mwamgeni Jongo.*

mbalimbali. Tunawashukuru sana na tunaomba ushirikiano huu uendelee kuwepo wakati wote," alisema Prof. Komba.

Kwa uapande wake, Katibu wa TSC, Paulina Nkwama alitumia mkutano huo kukemea vitendo

# TSC kushughulikia Watumishi wake wanaojihusisha na Rushwa







*Baadhi ya Washiriki wa mafunzo ya Kamati za TSC wa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa wakiwa katika hali ya utulivu wakati mafunzo yakiendelea.*

vya rushwa kwa watumishi wa Tume hiyo huku akieleza kuwa hatamvumilia yeyote atakayejihusisha na vitendo hivyo ambavyo vinaleta aibu kwa Taasisi anayoiongoza.

"Naomba kila mtumishi azingatie maadili ya kazi. Naibu Katibu Mkuu amezungumzia uwepo wa malalamiko ya wateja kuhusu baadhi ya watumishi. Mimi nitashirikiana na kila mtumishi anayefanya kazi yake kwa kuzingatia maadili ya kazi, lakini kwa yeyote atakayebainika kuhusika na vitendo vya rushwa nitakuwa mstari wa mbele kumchukulia hatua," alisema Nkwama.

Awali, akitoa maelezo ya utangulizi, Katibu huyo alieleza kuwa TSC imeweka utaratibu wa kutoa mafunzo kwa Kamati za Wilaya ili ziweze kutambua na kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi ili kutoka huduma bora kwa walimu.

Alifafanua kuwa moja ya majukumu ya Kamati za Wilaya ni kushughulikia mashauri ya nidhamu kwa walimu ambayo uendeleshaji wake unahitaji uelewa wa Sheria na Kanuni za TSC na za Utumishi wa Umma, hivyo ni muhimu kutoa mafunzo hayo ili waweze kutenda haki wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

"Tumetoa mafunzo haya kwenye kanda mbili, hii ni ya tatu, tumefikia Mikoa 12 na tumebakiwa na Mikoa 14. Mafunzo haya yamekuwa na faida sana katika utekelezaji wa majukumu ya Kamati. Hata ukiangalia kwenye uendeshaji wa mashauri ya nidhamu, kumekuwa na mabadiliko makubwa ikilinganishwa na siku za nyuma," alisema Nkwama.

Katika mafunzo hayo mada mbalimbali zilitolewa ikiwa ni pamoja na; majukumu ya TSC katika Ajira na Maendeleo ya Walimu, Maadili ya kazi ya ualimu, Mamlaka za Nidhamu na Rufaa kwa Walimu na majukumu yake, Taratibu za uendeshaji wa vikao vya Kamati za Wilaya, Muundo wa TSC pamoja na Historia ya TSC.

# TSC, UNICEF WAKUTANA KUJADILI MAENDELEO YA ELIMU

Uongozi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ukiongozwa na Mwenyekiti wa tume hiyo Prof. Willy Komba na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama Septemba 24, 2021 umekutana na kufanya mazungumzo na Wadau wa Maendeleo kutoka UNICEF kuhusu masuala mbalimbali ya maendeleo ya elimu nchini.



*Mwenyekiti wa TSC, Prof. Willy Komba akizungumza kwenye kikao kilichowakutanisha wadau wa maendeleo kutoka UNICEF kilichofanyika Septemba 24, 2021 jijini Dodoma. Pembeni yake ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*



*Mkuu wa Kitengo kinachoshughulikia masuala ya elimu kutoka UNICEF, Dk. Daniel Baheta akizungumza katika kikao kilichowakutanisha wadau wa maendeleo kutoka UNICEF na TSC kilichofanyika Septemba 24, 2021 jijini Dodoma. Pembeni yake ni Mkuu wa masuala ya Elimu wa UNICEF kwa Mkoa wa Dodoma, Pantalee Kapichi.*



*Maafisa kutoka TSC waliohudhuria kikao cha Wadau wa Maendeleo kutoka UNICEF kilichofanyika Septemba 24, 2021 jijini Dodoma.*



*Maafisa kutoka TSC waliohudhuria kikao cha Wadau wa Maendeleo kutoka UNICEF kilichofanyika Septemba 24, 2021 jijini Dodoma.*

# WALIMU BORA KATIKA NYANJA YA NIDHAMU, MAADILI, MIIKO NA UTOAJI ELIMU WENYE WELEDI KUPEWA TUZO YA HAMASA NA MOTISHA

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Ally Mwalimu (Mb), ameahidi kutoa tuzo kwa walimu bora nchini katika eneo la nidhamu, maadili, utendaji kazi katika utoaji wa elimu baada ya kupata mapendekezo ya vigezo vya utoaji tuzo hizo kutoka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) na kuona tuzo za TSC ili kutoa motisha na kuhamasisha walimu nchini kufanya vizuri zaidi.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) akiongea na Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi (hawapo pichani) wakati akifungua mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 katika ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Dodoma.*

Waziri Ummy aliyasema hayo Alhamis Septemba 09, 2021 akiwa Mgeni Rasmi katika hafla fupi ya ufunguzi wa Mkutano wa Baraza la Kwanza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Rais – Tume ya Utumishi wa Walimu (PO-TSC) kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Hazina, Treasury Square Jijini Dodoma.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (MB) wapili kutoka kushoto akiimba wimbo wa wafanyakazi (solidarity forever) wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma. Pichani, wa kwanza kutoka kushoto ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama na wa kwanza upande wa kulia ni Katibu wa Baraza hilo, Laurence Chankan akifuatiwa na Afisa kutoka TAMISEMI aliyeambatana na Waziri huyo.*

"Pamoja na changamoto kadhaa zilizopo natambua kuna walimu wapo maeneo mbalimbali hapa nchini ambao wanafanya vizuri katika kazi yao ya kutoa elimu kwa watoto wetu. Kwa uzito huo naunga mkono juhudi na wazo la Uongozi wa TSC la kutoa tuzo kwa mwalimu na walimu watakaoonekana au kubainika kuwa na sifa bora katika eneo la nidhamu, maadili, miiko na utekelezaji wenye weledi wa utoaji elimu na hii itakua baada ya kupata mapendekezo ya vigezo

# WALIMU BORA KATIKA NYANJA YA NIDHAMU, MAADILI, MIIKO NA UTOAJI ELIMU WENYE WELEDI KUPEWA TUZO YA HAMASA NA MOTISHA



*Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wakiimba wimbo wa mshikamano wakati wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

vya utoaji tuzo hizo kutoka TSC na kuona tuzo za TSC ili kutoa motisha na kuhamasisha walimu nchini kufanya vizuri zaidi." Alisema Waziri Ummy.

Pamoja na kuunga mkono jitihada hizo za kutoa motisha na kujitahidi kuendelea kutatua changamoto mbalimbali za walimu, ameelekeza walimu kuacha kutumikisha wanafunzi katika miradi ya maendeleo shuleni kama ujenzi wa miundombinu ya shule kama; vyoo n.k ili kuwapa fursa ya kufanya na kutekeleza kilichowapeleka shuleni kwani Serikali inatoa fedha nyingi katika utekelezxaji wa miradi hiyo.

Wakati huohuo Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Mwalimu Paulina Nkwama aliipongeza Serikali kwa kuajiri Walimu 14,949 katika Mwaka wa Fedha 2020/21 na kuwapandisha vyeo watumishi wakiwemo walimu 126,346 na kati yao 121,663 sawa na asilimia 96.2 wamepata mshahara mpya hali iliyosaidia kupunguza malalamiko, kuongeza tija na ufanisi na hivyo kuinua kiwango cha elimu nchini.

Alisema, pamoja na ufinyu wa bajeti unaoikabili Tume, katika kipindi cha miaka mitano tangu Tume ilipoanza kutekeleza majukumu yake mwezi Julai, 2016 kwa kushirikiana na OR-TAMISEMI pamoja na wadau wake imefanikiwa kuajiri walimu 33,522; walimu 28,886 (86%) walisajiliwa kati ya 33,522 walioajiriwa, walimu 4,636 (14%) ambao ni ajira ya mwezi Juni, 2021 wanaendelea kusajiliwa; walimu 26,573 (92%) walithibitishwa kazini kati ya 28,886 waliosajiliwa na walimu 6,949 hawajatimiza vigezo vya kuthibitishwa.

Aliongeza kuwa walimu 215,813 walipandishwa vyeo; walimu 11,149 walibadilishwa cheo baada ya kujiendeleza kielimu; walimu 27,925 waliandikiwa vibali vya kustaafu kazi, hali kadhalika Tume pia imeshughulikia Mafao ya Walimu 2,105 ya kabla ya Julai 01, 2004 yanayohusu Pensheni, Mirathi na Mikataba na kulipwa na Hazina.

Aidha, Katibu huyo alisema katika kipindi hicho cha miaka mitano (2016/17 – 2020/21), Tume ilitoa uamuzi wa mashauri



*Wajumbe wa Baraza la wafanyakazi wakiimba wimbo wa mshikamano wakati wa Mkutano wa Baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

# WALIMU BORA KATIKA NYANJA YA NIDHAMU, MAADILI, MIIKO NA UTOAJI ELIMU WENYE WELEDI KUPEWA TUZO YA HAMASA NA MOTISHA

ya nidhamu 10,479 (95%) kati ya 10,978 yaliyoanzishwa. Kati ya mashauri hayo 6,891 (66%) yalihusu utoro, makosa mengine ni uzembe kazini walimu 56 (0.5%), ulevi 66 (0.6%), mahusiano ya kimapenzi na wanafunzi 285 (2.7%), kughushi 1,723 (16.4%), kukiuka maadili ya Kazi ya Ualimu 1,290 (12.3%).

"Hadi sasa rufaa za Walimu 738 (88%) kati ya 834 zimetolewa uamuzi. Ni rufaa 96 (12%) zilizobaki, ambapo kati ya hizo; 54 zimeandaliwa kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Tume utakaofanyika Septemba 22, 2021, rufaa 24 zipo katika hatua ya uchambuzi na 18 zinasubiri vielelezo kutoka Wilayani."



*Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu wakiwa katika Mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi na viongozi wengine mara baada ya kufungua mkutano wa baraza hilo Septemba 9, 2021, jijini Dodoma. Pichani, kushoto kwa Waziri ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama.*

# WALIMU BORA KATIKA NYANJA YA NIDHAMU, MAADILI, MIIKO NA UTOAJI ELIMU WENYE WELEDI KUPEWA TUZO YA HAMASA NA MOTISHA

Alisema Mwalimu Nkwama.

Akizungumzia ziara za mara kwa mara katika Ofisi za Tume za Wilaya alisema Tume imefanya ziara kwenye wilaya zote 139 (100%) kuitangaza Tume na kuwaelimisha wadau kufahamu majukumu ya Tume ikiwa ni pamoja na ufuatiliaji wa utekelezaji wa majukumu ya Tume uliofanyika katika mwaka wa fedha 2020/21 ambapo Ofisi za Wilaya 78 (56%) kati ya 139 zimewezeshwa kufanya ziara shuleni kuwaelimisha walimu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu, Maadili/ Miiko ya Ualimu, Haki na Wajibu wa Mwalimu na wilaya 61 (44%) zilizobaki ilielezwa zitaendelea kuwezeshwa kufanya ziara hizo kwa kadri Bajeti itakavyoruhusu.

Akitoa neno la shukrani kwa Mgeni Rasmi, mwakilishi wa Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi kwa niaba ya Watumishi wote wa Tume ya Utumishi wa Walimu Ndg. Nuhu Mlekwa alikiri kupokea maelekezo na kuahidi kuyazingatia yote katika utekelezaji wake kwa kushirikiana na Serikali hasa eneo la uratibu na usimamizi wa utoaji ajira kwa walimu na kuwatembelea katika maeneo yao ya kazi kupeana elimu zaidi ya maadili, miiko na nidhamu ya kazi ya ualimu na kubaini changamoto zinazojitokeza ili kupata ufumbuzi wa pamoja.



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (wa tatu kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wakati wa Mkutano wa baraza hilo uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

# WALIMU WA SEKONDARI ARUSHA JIJI WAPONGEZWA NA KUPEWA MOTISHA KWA UFAULU MZURI WA WANAFUNZI WAO



*Mkuu wa Shule ya Sekondari Kinana, Mwl. Desdery Cyprian Kabulika, akipokea cheti na zawadi kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ephraim Simbeye katika hafla ya kuwapongeza walimu waliofaulisha wanafunzi vizuri. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Arusha.*

**Na. Mwandishi Wetu – Arusha Jiji**

Mkurugenzi wa Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) Ndg. Ephraim Simbeye, amewapongeza na kukabidhi vyeti na zawadi mbalimbali kwa walimu wote wa Shule za Sekondari za Serikali na Binafsi mkoani Arusha kwa jitihada wanazofanya katika kutoa elimu na mafunzo stahiki kwa wanafunzi hali iliyowezesha kuwa na mabadiliko makubwa katika matokeo ya mitihani ya Taifa ya kidato cha pili na kidato cha nne mwaka 2020.

Hafla hiyo ya pongezi na makabidhiano ilifanyika hivi karibuni jijini Arusha katika ukumbi wa hafla mbalimbali Pallot ambapo pamoja na motisha zilizokabidhiwa kwa walimu husika Ndg. Simbeye aliwapongeza na kuwashukuru walimu wote kwa jitihada mahususi za kuongeza kiwango cha ufaulu mwaka hadi mwaka na kuwasisitiza waongeze bidii zaidi ili kuendelea kuinua kiwango cha ufaulu.

Ndg.Simbeye ambaye katika hafla hii alikua Mgeni Rasmi alitoa zawadi kwa shule zote zilizofanya vizuri kuanzia iliyoshika nafasi ya kwanza hadi ya tatu pamoja na walimu wote waliowezesha wanafunzi wao kufaulu katika mitihani tajwa ikiwa ni vyeti pamoja na fedha taslimu.

Aidha, katika hafla hiyo Mkurugenzi Simbeye pia alikabidhi vyeti vya pongezi kwa walimu na watumishi wengine waliohudumu katika sekta ya elimu kwa utumishi uliotukuka ikiwa ni pamoja na kuendelea kuwasisitiza kudumisha uzalendo katika usimamizi wa taaluma shuleni na maeneo mengine ya kisekta katika jamii zetu nchini.

Wakati huohuo nae Kaimu Katibu Msaidizi wa Arusha Jiji Ndg.



*Mwl. Zuhura Mringo akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ephraim Simbeye katika hafla ya kuwapongeza walimu waliofaulisha wanafunzi vizuri. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Arusha.*

## WALIMU WA SEKONDARI ARUSHA JIJI WAPONGEZWA NA KUPEWA MOTISHA KWA UFAULU MZURI WA WANAFUNZI WAO



*Mwl. Elisa B. Mkwizu wa Shule ya Sekondari Arusha (Somo la Biolojia) akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ephraim Simbeye katika hafla ya kuwapongeza walimu waliofaulisha wanafunzi vizuri. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Arusha.*



*Mwl. Abinuth Mohamed Marekero ambaye amestaafu akipokea cheti cha pongezi kutoka kwa Mkurugenzi wa Elimu Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI), Ephraim Simbeye katika hafla ya kuwapongeza walimu waliofaulisha wanafunzi vizuri. Hafla hiyo ilifanyika hivi karibuni jijini Arusha.*

Joyce Macha kwa niaba ya walimu mkoani humo aliahidi kuendelea kusimamia kwa weledi utoaji elimu kwa wanafunzi na kufanya kazi kwa bidii zaidi ili kuinua zaidi kiwango cha taaluma mkoani humo.

Alisema kuwa shule zilizofanya vizuri katika mitihani ya Taifa kwa kidato cha nne mwaka 2020 katika Jiji la Arusha ni pamoja na Shule ya Sekondari ya Kutwa ya Arusha, Shule ya Sekondari Kimaseki, Shule ya Sekondari Felix Mrema huku shule iliyoongeza ufaulu kutoka chini kwenda juu ni Shule ya Sekondari Kinana.

Kaimu Katibu Msaidizi huyo alisema wakuu wa shule zilizofanya vizuri ni pamoja na Mwalimu Lyidia Eliakimu Kikura ambaye ni Mkuu wa Shule ya Kutwa ya Sekondari Arusha, Mwalimu Joseph Manase Maro ambaye ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Kimaseki, Mwalimu Reginald Yohana Msendekwa wa Shule ya Sekondari Felix Mrema, na Mwalimu Desdery Cyprian Kabulika



*Walimu wakimshangilia mwenzao baada ya kupokea cheti cha pongezi.*



*Walimu wakiwa katika hafla ya kujipongeza kwa kufaulisha wanafunzi vizuri.*

## WALIMU WA SEKONDARI ARUSHA JIJI WAPONGEZWA NA KUPEWA MOTISHA KWA UFAULU MZURI WA WANAFUNZI WAO



*Walimu wakiserebuka wakati hafla ya kupongezwa kwao kwa kufaulisha wanafunzi katika masomo mbalimbali.*

ambaye pia ni Mkuu wa Shule ya Sekondari Kinana.

Vilevile Ndg. Macha alisema walimu waliofanya vizuri katika masomo mbalimbali ni pamoja na; Mwl. Judith Mwangalika William, Shule ya Sekondari Moshono (Somo la Historia), Mwl. Walter Marishani, Shule ya Sekondari Felix Mrema (Somo la Kiswahili), Mwl. Elisa B. Mkwizu, Shule ya Kutwa ya Sekondari Arusha (Somo la Biolojia), Mwl. Charles Meppo, Shule ya Sekondari Kimaseki (Somo la Hesabu), Mwl. Owen Mwambene, Shule ya Sekondari Njiro (Somo la Hesabu); na Mwl. Venance Nkungu, Shule ya Sekondari Felix Mrema (Somo la Fizikia) wakati Mwl. Zuhura Mringo, Afisa Elimu Kata akipongezwa kwa kata yake kufanya vizuri.

Kaimu Katibu Msaidizi aliwataja wengine waliotunukiwa utukuka na pongezi za mafanikio kuwa ni pamoja na Mwalimu Mstaafu Abinuth Mohamed Marekero na Mwl. Valentine Makuka, Afisa Elimu Sekondari Arusha Jiji.

Wawezeshaji katika hafla hiyo walikua ni Mkurugenzi wa Jiji la Arusha, Chama Cha Walimu Tanzania (CWT), Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), na wadau wengine wa walimu.



*Walimu wakiserebuka wakati hafla ya kupongezwa kwao kwa kufaulisha wanafunzi katika masomo mbalimbali.*

# NAIBU KATIBU MKUU MWELI AMEITAKA TSC KUKAMILISHA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA KWA WAKATI



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli (kushoto) akiwa pamoja na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama wakati wa Mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringia yaliyofanyika Septemba 20 na 21 katika Ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

**Na. Mwandishi Wetu - Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli, ameitaka Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuharakisha ukamilishaji wa kituo cha huduma kwa wateja (Clients Service Center) ili walimu waweze kuwasilisha malalamiko, maoni, ushauri na hoja ikiwa ni moja ya njia za kuboresha utoaji wa huduma kwa walimu.

Ndg. Mweli aliyasema hayo hivi karibuni akiwa Mgeni Rasmi katika Ufunguzi wa Kikao Kazi cha Mafunzo ya Kamati za Wilaya za Kanda ya Kati inayojumuisha Mikoa ya Dodoma, Iringa, Singida, na Manyara kilichofanyika Chuo cha Mipango, jijini Dodoma.

"Ofisi ya Rais – TAMISEMI inafanya kazi kwa karibu sana na TSC katika kushughulikia masuala yote ya utumishi wa walimu na ndiyo maana tayari TAMISEMI ina mfumo wa kupokea malalamiko ya wateja wake. Hivyo naielekeza TSC kuharakisha ukamilishaji wa kituo cha huduma kwa wateja (Clients Service Center) ndani ya Tume ili walimu waweze kuwasilisha hoja zao na kupatiwa huduma kwa urahisi na kwa haraka." Alisema Naibu Katibu Mkuu Mweli.

Aidha Mweli alisema TSC ni chombo muhimu katika sekta ya elimu na hivyo ni lazima kuendelea kujengeana uwezo, kuwezeshana kirasilimali na miundombinu kwani kwa uchache yamesaidia kupunguza idadi ya mashauri ya rufaa za walimu zinazoshinda kutoka 43 mpaka tatu kwa zile zilizowasilishwa Makao Makuu ya TSC.

Aliongeza kuwa TAMISEMI kwa kushirikiana na TSC inatafuta fedha ili kukamilisha kwa haraka mfumo wa taarifa za walimu ambao moduli tatu kati ya sita zimeshakamilika na kufanyiwa majaribio hivyo mara baada ya kukamilika kwake kila taarifa muhimu ya mwalimu lazima iwemo humo.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Mgeni Rasmi, Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu Prof. Willy Komba, alimshukuru Mgeni Rasmi ambaye ni Naibu Katibu Mkuu (Elimu) Ndg. Gerald Mweli kwa kusukuma na kusimamia ipaswavyo zoezi la upandishwaji madaraja na vyeo vya walimu kwa wakati.





*Baadhi ya Washiriki wa mafunzo ya Kamati za TSC wa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa wakiwa katika hali ya utulivu wakati mafunzo yakiendelea.*

# NAIBU KATIBU MKUU MWELI AMEITAKA TSC KUKAMILISHA KITUO CHA HUDUMA KWA WATEJA KWA WAKATI



*Mkurugenzi wa Kitengo cha Huduma za Sheria kutoka TSC, Wakili Richard Odongo akiwasilisha mada kuhusu taratibu za uendeshaji wa mashauri ya nidhamu ya walimu wakati wa mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika kwa siku mbili katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*



*Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani, Grace Mrema (wa kwanza kutoka kulia), Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Moses Chitama (wa pili kutoka kulia), Mkurugenzi wa Ajira Maadili na Maendeleo ya Walimu, Christina Hape (wa tatu kutoka kulia) na Mkuu wa Kitengo cha Mipango Ufuatiliaji na Tathmini, Evodia Pangani wote kutoka TSC Makao Makuu wakiwa katika picha ya pamoja wakati wa mafunzo ya Kamati za TSC yaliyofanyika hivi karibuni katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*

Nae Katibu wa TSC Mwl. Paulina Nkwama alisema kikao kazi cha mafunzo hayo kinafanyika ili kuwajengea uwezo wajumbe wa kamati za wilaya kwa kanda ya kati na kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufasaha na ufanisi mkubwa zaidi ikiwa ni pamoja na kutambua wajibu na majukumu yao.

"Mashauri ya rufaa yanayowasilishwa makao makuu ya TSC hivi sasa ni chini ya asilimia 10 na kati ya hizo asilimia 90 maamuzi yake yaliyofanywa wiliayani huwa ni maamuzi sahihi yasiyo na shaka na hii inaonyesha bayana kamati zinafanya kazi na maamuzi sahihi kwa mujibu wa miongozo, kanuni na taratibu zilizowekwa katika kushughulikia masuala ya utumishi wa walimu wilayani." Alisema Mwl. Nkwama.



*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Miko na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mafunzo ya Kamati za TSC za Wilaya yaliyofanyika katika Chuo cha Mipango jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba akifunga Mafunzo ya Kamati za TSC kwa Wilaya za Mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Iringa yaliyofanyika Septemba 20 na 21 katika Chuo cha Mipango jijini Dodoma. Pembeni yake ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama.*

# Waziri Ummy akutana na Menejimenti ya TSC

**Na Mwandishi Wetu.**

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu amekutana na Menejimeti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) ikiwa ni mara ya kwanza tangu alipoteuliwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan katika nafasi hiyo.

Mkutano huo ulifanyika Septemba 7, 2021 katika Ukumbi wa TSC jijini Dodoma ambapo mambo mbalimbali yalijadiliwa huku suala la masomo ya ziada (tuition) kwa wanafunzi wa shule za msingi na uhusiano wa mapenzi kati ya walimu na wanafunzi vikitawala mkutano huo.

Waziri huyo alieleza kuwa kumekuwa na wimbi la wazazi kuchangishwa fedha na walimu kwa ajili ya kuwafundisha masomo ya ziada (tuition) wanafunzi wa shule za msingi kitu ambacho kinasababisha watoto hao kukosa muda wa kufanya mambo mengine ya kijamii.

"Siku hizi watoto wa darasa la pili wana tuition hii siyo sawa kabisa. Unakuta mtoto kuanzia asubuhi hadi usiku ni shule tu hana hata muda wa kuwasaidia wazazi shughuli ndogondogo, na walimu hawa wamekuwa wakiwashawishi wazazi kuchanga fedha kwa ajili ya hizo tuition. Kuna sehemu zingine unakuta watoto hawa wanafundishwa hadi usiku kitu ambacho siyo salama," alisema Waziri Ummy.

Kutokana na hilo, Waziri huyo



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kulia) akipokea ua kutoka kwa mtumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Enid Geofrey mara baada ya kuwasili katika ofisi za TSC.*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (kushoto) akiwa pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama mara baada ya kufika kwenye ofisi za TSC kwa ajili ya kufanya kikao na Menejimenti ya tume hiyo.*

alieleza kwamba anatarajia kukutana na Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia kwa ajili ya kuona namna ya kusitisha jambo hilo kwani hakuna haja ya kuwepo kwa masomo ya ziada kwa watoto hao endapo walimu wanawajibika ipasavyo.

Kwa upande wa uhusiano wa mapenzi kati ya walimu na wanafunzi, Ummy alieleza kuwa Tume hiyo haipaswi kumwonea huruma mwalimu yeyote atakayebainika kuwa na tabia hizo ili kuwalinda wanafunzi na kuhakikisha wanatimiza ndoto zao.

"Katika suala la mapenzi na wanafunzi ninawataka msimwonee huruma mwalimu

# Waziri Ummy akutana na Menejimenti ya TSC

yeyote hata kidogo, hili nalizungumza nikiwa kama Waziri lakini pia nikiwa kama mama. Walimu wenye tabia hiyo mkiwafukuza kazi alafu baada ya mwaka mmoja wakileta maombi ya kutaka kuajiriwa tena msiwakubalie," alisisitiza Waziri.

Pamoja na hayo Waziri ummy aliitaka TSC kuahikisha inatoa elimu kwa walimu ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi na pale inapotokea mwalimu anachukuliwa hatua za nidhamu Tume hiyo isimamie katika kutenda haki kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Waziri Ummy aliipongeza Tume kwa kufanya kazi kwa bidi katika kusimamia Ajira, Maadili na maendeleo ya walimu huku akieleza kuwa TSC ni chombo muhimu ambacho kinategemewa katika kuleta ustawi wa walimu na maendeleo katika sekta ya elimu.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu akisaini kitabu cha wageni akiwa katika ukumbi wa Mikutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC).*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo katika kikao cha Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu na Menejimenti ya TSC kilichofanyika septemba 7, 2021.*



*Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Paulina Nkwama (kushoto) akimkabidhi Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Tume hiyo wakati wa kikao cha Waziri huyo na Menejimenti ya TSC kilichofanyika Septemba 7, 2021.*



*Wajumbe wa kikao cha Menejimenti ya TSC wakiwa katika kikao na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu.*

# MWENYEKITI TUME YA UTUMISHI WA WALIMU PROF. KOMBA AWAKUMBUSHA NGUZO KUU ZA MAADILI WALIMU SHULE YA SEKONDARI LIPUPUMA, SONGEA



*Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba.*

**Na. Mwandishi Wetu.**

Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba amewakumbusha walimu wa shule ya sekondari Lipupuma, Songea wajibu na nguzo kuu za maadili ya walimu ikiwemo; wajibu wao kwa mtoto (mwanafunzi), wajibu wa kazi yao kama walimu, wajibu wao kwa mwajri, wajibu wao kwa jamii, na wajibu wao kwa Taifa la Tanzania.

Mwenyekiti aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa kikao kazi cha Tume ya Utumishi wa Walimu Makao Makuu na walimu wa Shule ya Sekondari Lipupuma, wilayani Songea kilichofanyika shuleni hapo.

"Kipengele cha wajibu wetu kama walimu kina nguzo kuu tano ambazo tunawajibika kuzizingatia sana katika utumishi wetu kama walimu na kama watumishi wa umma. Nguzo hizo ni pamoja na wajibu wetu kwa watoto ambao ndiyo wanafunzi wetu; wajibu wa kazi yetu ambayo ni kufundisha watoto darasani na nje ya darasa ikiwa ni pamoja na kuwafunza nidhamu, maadili, stadi za kazi, utii, n.k; lakini pia wajibu wetu kwa mwajiri ambaye ni Serikali kupitia OR-TAMISEMI na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia; nguzo ya nne ni wajibu wetu kwa jamii tunayoihudumia na inayotuzunguka popote tuwapo; na mwisho ni wajibu wetu kwa Taifa la Tanzania." Alisema Prof. Komba

Mwenyekiti alisema TSC ni chombo muhimu kwani ndilo kimbilio la walimu katika masuala mbalimbali ya ajira, nidhami na maadili katika utumishi wa umma kwani pia inasaidia katika kurekebisha tabia na kulinda maadili ya walimu kupitia mashauri mbalimbali ya kinidhamu yanayowasilishwa ili kuyapatia ufumbuzi na suluhisho la pamoja.

Prof.Komba alisema muundo wa Tume umeundwa kwa mujibu wa Sheria iliyounda Tume ambao unajumuisha Mwenyekiti na Katibu wa Tume wanaoteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Wajumbe wa Kamati (Makamishna) ambao ni wateule wa Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; pamoja na Makatibu Wasaidizi ambao wapo katika wilaya zote 139 Tanzania Bara wanaoteuliwa na Katibu wa Tume.

Nae Mwalimu Veronica Pango akitoa shukrani kwa niaba ya walimu waliohudhuria kikao kazi hicho alisema, wamepokea maelekezo yote kwa ajili ya kuyafanyia kazi kwani wajumbe wameonyesha kuelewa zaidi wajibu wao na kukubaliana kutekeleza kwa weledi na ufanisi zaidi.

# Wajumbe wa Kamati ya Bunge waahidi kuongeza Bajeti ya TSC

**Na. Mwandishi Wetu.**

Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) wameridhishwa na utendaji kazi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika kusimamia ajira, maadili na maendeleo ya walimu nchini na hivyo kuahidi kushawishi wabunge wenzao ili kuongeza bajeti ya Tume hiyo.

Wajumbe wa kamati hiyo ambao ni Mbunge wa Jimbo la Wingwi, Mhe. Omar Issa Kombo na Mbunge wa Viti Maalum, Mhe. Mwantum Zodo waliyasema hayo wakati wa halfla ya kukabidhi pikipiki 74 kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC iliyofanyika mapema mwezi Septemba, 2021 katika ofisi za Tume hiyo jijini Dodoma.

Akizungumza katika hafla hiyo ambayo mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, Mhe. Kombo alieleza kuwa TSC imefanya kazi kubwa katika kusimamia maadili ya walimu pamoja na masuala mbalimbali yanayohusu maendeleo yao.

Alisema kuwa pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika, bajeti ya Tume hiyo ni ndogo ikilinganishwa na majukumu yanayotakiwa kutekelezwa katika kutoa huduma kwa walimu, hivyo aliahidi kuwa itakapofika kipindi cha bajeti kamati hiyo itahakikisha



*Mbunge wa Jimbo la Wingwi na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Omar Issa Kombo akiongea na wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (hawapo pichani) katika ukumbi wa Mikutano wa Tume hiyo jijini Dodoma.*



*Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Mwantum Zodo akiongea na wajumbe wa Menejimenti ya Tume ya Utumishi wa Walimu (hawapo pichani) katika ukumbi wa Mikutano wa tume hiyo jijini Dodoma.*

# Wajumbe wa Kamati ya Bunge waahidi kuongeza Bajeti ya TSC

TSC inaongezewa fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

"Mhe. Waziri kwanza napenda niseme kuwa nimefurahi sana kuambatana na wewe katika hafla hii ya kukabidhi pikipiki kwa Kaimu Katibu wa Wasaidizi ili wakatekeleze majukumu yao kwa ufanisi zaidi. Nakiri kwamba leo nimejifunza mambo mengi ambayo nilikuwa siyajui kuhusu utendaji wa Tume hii. Nimeona TSC imepewa majukumu makubwa kwa majibu wa sheria lakini ukiangalia bajeti yake haiendani na majukumu hayo," alisema Mhe. Kombo.

Mbunge huyo anaendelea kusema kuwa "TSC ikiwezeshwa na kutekeleza majukumu yake vizuri ni wazi kuwa walimu wetu watapata huduma bora, na wao watatekeleza vizuri wajibu wao wa kufundisha. Hivyo, napenda niahidi kuwa suala la ufinyu wa bajeti kwa Tume tunalichukua na tutaliwasilisha kwenye kamati yetu ili wakati utakapofika tuhakikishe bajeti ya TSC inaongezwa."

Kwa upande wake Mhe. Zodo alieleza kuwa TSC imepiga hatua katika kutoa elimu kwa walimu ili waweze kuwa na uelewa wa kutosha juu ya Sheria, Kanuni na Taratibu za kiutumishi na waweze kuzingatia wakati wote wakiwa shuleni au hata nje ya shule.

Aliongeza kuwa pamoja na jitihada kubwa ambazo TSC imezifanya, bado kuna uhitaji mkubwa wa kuendelea kuwafikia walimu na kuwasaidia kutatua kero zao ili na wao waweze kufundisha wanafunzi wakiwa na amani.

"Mhe. Waziri naungana na mbunge mwenzangu kupongeza kazi kubwa inayofanywa na Tume hii. Kwa kweli ninaona kuna haja ya TSC kuongezewa bajeti ili itekeleze majukumu yake kwa ufanisi. Naomba nikuahidi kuwa itakapofikia kujadili bajeti ya TSC lazima tufanye kila linalowezekana kuhakikisha tunaongeza bajeti hapa ili watoto wetu waendelee kuwa salama wawapo shuleni," alisema Zodo.

Mbunge huyo alisema kuwa pamoja na kwamba bado kuna changamoto mbalimbali zinazowakabili walimu, kwa kiasi kikubwa TSC imesaidia kutatua kero hizo hususan katika eneo la upandishaji madaraja ambapo walimu wengi waliokuwa na sifa za kupanda walipandishwa kwa wakati na 96% ya waliopanda wamebadilishiwa mishahara yao.



*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Seikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (kushoto) akiongea jambo na Mbunge wa Viti Maalum na Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mhe. Mwantum Zodo wakati wa hafla ya kukabidhi pikipiki kwa Kaimu Makatibu Wasaidizi wa TSC iliyofanyika Septemba 7, 2021 jijini Dodoma.*

# KONGOLE TSC KUSHUGHULIKIA KWA WELEDI NA UWAZI MASHAURI YA WALIMU NCHINI - NAIBU KATIBU MKUU (ELIMU) OR – TAMISEMI




*Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) anayeshughulikia elimu, Gerald Mweli (katikati) akiwa na Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC), Prof. Willy Komba (kushoto) pamoja na Katibu wa TSC, Paulina Nkwama. Naibu Katibu Mkuu huyo alitembelea Mkutano wa Tume hivi karibuni ili kujionea namna Tume hiyo inavyoshughulikia rufaa za walimu.*

**Na Mwandishi Wetu.**
**Dodoma**

Naibu Katibu Mkuu anayeshughulikia Elimu kutoka Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ndg. Gerald Mweli, ameipongeza Tume ya Utumishi wa Walimu kwa kushughulikia kwa weledi na uwazi rufaa za walimu hapa nchini kwa uwepo na ujumuishwaji wa vielelezo bayana vya mashauri ya walimu waliotuhumiwa kukengeuka kimaadili katika utumishi wa walimu.

Ndg. Mweli aliyasema hayo hivi karibuni alipokua akizungumza na Makamishna na Sekretarieti ya Tume waliokua wakiendesha Mkutano wa Tume wa Kwanza kwa Mwaka wa Fedha 2021/ 2022 uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Jijini Dodoma.

"Nawapongeza sana Makamishna na Sekretarieti yenu (Tume) kwa kushughulikia kwa weledi na uwazi masuala na mashauri ya walimu hapa nchini. Uwepo na ujumuishwaji wa vielelezo bayana vya mashauri ya walimu waliotuhumiwa kukengeuka kimaadili katika utumishi wa walimu na utumishi wa umma kwa ujumla wake ni wazi inathibitisha usawa na uhalali wa maamuzi mnayofanya juu ya mashauri mbalimbali ya walimu wetu hapa nchini kwa



*Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu ukiwa unaendelea.*

# KONGOLE TSC KUSHUGHULIKIA KWA WELEDI NA UWAZI MASHAURI YA WALIMU NCHINI - NAIBU KATIBU MKUU (ELIMU) OR – TAMISEMI

niaba ya Serikali." Alisema Naibu Katibu Mkuu Mweli

Mweli alishauri kuwa pamoja na kazi kubwa na nzuri inayofanywa na Tume, basi ni vema mafunzo yanayofanyika kuwajengea uwezo Makatibu Wasaidizi waliopo wilayani yafanyike pia kwa pande zote mbili pamoja na walimu ambao ndiyo wahusika wakuu kwa Tume ili nao wazidi kutambua miongozo mbalimbali ya taaluma yao, Sheria, Kanuni, Taratibu, Maadili, Nidhamu na Miiko ya kazi ya ualimu na utumishi wa umma.

Pamoja na kuunga mkono jitihada hizo za kazi zinazofanywa na Tume, aliahidi kuendelea kuwa balozi wa Tume katika maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutumia vikao vya Wakurugenzi wa Manispaa, Halmashauri za Wilaya na Miji kukazia suala la kuyachukulia kwa uzito mkubwa zaidi na uangalifu unaostahili kwa kushirikisha mamlaka zote zinazohusika ikiwemo Tume katika maamuzi ya masuala mbalimbali ya walimu katika wilaya na halmashauri zao hapa nchini.

Aidha Mwenyekiti wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Prof. Willy Komba alimshukuru kwa ushuhuda huo na ahadi ya kuwa balozi wa Tume katika mikutano na vikao mbalimbali vya kikazi ili kuongeza ufanisi zaidi wa utekelezaji wa majukumu ya Tume.



*Mkutano wa Tume ya Utumishi wa Walimu ukiwa unaendelea.*

# CHANKAN, LEMUNGE WATETEA NAFASI ZAO BARAZA LA WAFANYAKAZI

Na Mwandishi Wetu

Baraza la Wafanyakazi la Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) limefanya uchaguzi wa Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza hilo ambapo Laurence Chankan na Neema Lemunge walifanikiwa kuteteza nafasi zao kwa awamu ya pili.

Uchaguzi huo uliofanyika Septemba 9, 2021 wakati wa mkutano wa baraza hilo uliofanyika katika Ukumbi wa Wizara ya Fedha na Mipango jijini Dodoma ambapo mwenyekiti wa Baraza hilo ambaye pia ni Katibu wa TSC, Paulina Nkwama aliwasilisha majina ya watumishi walipendekezwa na menejimenti ya Tume ili waweze kupigiwa kura.

Majina yaliyowasilishwa ni Neema Lemunge, Laurance Chankan na Ramadhani Ngaegela wote kutoka Idara ya Ajira, Maadili na Maendeleo ya Walimu pamoja na Jenipha Maagi kutoka Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu.

Katika matokeo ya kura hizo,



*Katibu wa Baraza la Wafanyakazi, Laurence Chankan akitoa neno la shukrani mara baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo kwa awamu ya pili.*



*Katibu Msaidizi wa Baraza la Wafanyakazi, Neema Lemunge akitoa neno la shukrani mara baada ya kuchaguliwa kushika nafasi hiyo kwa awamu ya pili.*



*Mkurugenzi Msaidizi Anayesimamia Utawala kutoka TSC, Apsa Othman akitoa maelezo mafupi kabla ya kufanyika kwa uchaguzi wa Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza hilo la TSC wakati wa Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

# CHANKAN, LEMUNGE WATETEA NAFASI ZAO BARAZA LA WAFANYAKAZI



*Maafisa wakiendelea na zoezi la kuhesabu kura za nafasi ya Katibu na Katibu Msaidizi wa Baraza hilo wakati wa uchaguzi uliofanyika Septemba 9, 2021 jijini Dodoma.*

Lawrence Chankan alitangazwa kuwa Katibu wa Baraza hilo baada ya kuibuka na ushindi kwa kupata kura19 kati ya 55 huku Neema Lemunge akishika nafasi ya Katibu Msaidizi kwa kushika nafasi ya pili kwa kupata kura15 kati ya 55.

Wawili hao wanatumikia nafasi hizo kwa awamu ya pili ambapo kwa mujibu wa taratibu zinazoongoza chombo hicho, uchaguzi wa Baraza la wafanyakazi hufanyika kila baada ya miaka mitatu.

Kabla ya kufanyika kwa mkutano huo, ulifanyika uchaguzi wa kuwapata wajumbe wanaounda baraza la sasa kutoka Tume Makao Makuu na wilayani ambapo kwa mujibu wa taratibu wajumbe hao ndio wenye wajibu wa kuwasilisha hoja za watumishi katika mikutano ya baraza la wafanyakazi ili Menejimenti iweze kutoa majibu.







*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Mhe. Ummy Mwalimu (katikati kwa waliokaa) akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi na viongozi wengine mara baada ya kufungua mkutano wa baraza hilo Septemba 9, 2021, jijini Dodoma. Pichani, kushoto kwa Waziri ni Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu, Paulina Nkwama.*



**MAWASILIANO:** Katibu, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mtaa wa Mtendeni S.L.P 353, DODOMA
**Simu: +255 (26) 2322402-4** **Barua Pepe:** *secretary@tsc.go.tz* **Tovuti:** *www.tsc.go.tz*

***Tume ya Utumishi wa Walimu Tanzania*** ***tumeyautumishiwawalimutanzania***